

# Uchumi na BIASHARA

12 OXFAM INAVYOLETA MPANGO WA KUSAIDIA JAMII UWEKEZAJI WA ARDHI



Mkuu wa mkoa wa Kagera, Marco Gaguti (katikati mwenye shati jeupe) akizindua msimu wa kahawa.

## Wakulima wa kahawa wanavyopoteza mapato kwa kutobadili mbinu

Na Diana Deus

**K**ILIMO cha kahawa mkoani Kagera ni kilimo kikongwe kinachoendelezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kama kilimo biashara.

Pamoja na uwepo wa mashamba mapya ya kahawa yanayozishwa, idadi kubwa imekuwa ni mashamba ya kurithishana kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine.

Mara nyingi, baba anapofariki dunia shamba la kahawa hurithiwa na watoto ili kuliendeleze na mara nyingi kwa mila za watu wa Kagera, mtoto mwenye matendo mazuri kwa wazazi wake ndiye hupewa kipaumbele cha kurithi shamba la mibuni.

Kwa sasa kuna dhana kwamba huenda mwenendo wa kurithi mashamba ya kahawa umechangia kupunguza uzalishaji wa zao hilo